WiLDAF-TZ



# UONGOZI

# UONGOZI NI NINI?

Uongozi maana yake ni mchakato unaoweza kushawishi jamii, kikundi cha watu kufanya shughuli iliyopangwa ili kufikia malengo yaliyowekwa. **(Kruse 2013; Kouzes 1987; Northouse 2007)**

Kwa tafsiri nyingine uongozi ni uwezo wa kutekeleza dira. Hivyo kiongozi anahitaji awe na uwezo, utashi wa kuunganisha watu kuelekea lengo la pamoja. Vilevile kiongozi anahitajika awe na sifa ya kujiamini na kuaminiwa.

Uongozi wa kisiasa hauna tofauti na uongozi mwingine bali uhusisha zaidi kushika nafasi mbalimbali za uongozi wa kisiasa katika ngazi za vijiji vitongoji, kata n.k.
Ni vyema kuzingatia kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 1992, uongozi wa kisiasa ni moja ya mlango mkubwa na njia muhimu ya kuwa kiongozi ili kuwa na fursa ya kutoa maamuzi katika nchi yetu.



# AINA ZA UONGOZI

*Kuna aina kuu mbili za uongozi*

1. **Kidemokrasia**
   kiongozi hupatikana kupitia uchaguzi huru, wa haki na unaoaminika.

2. **Kimabavu**
   kiongozi hupatikana kwa njia zisizo za kidemokrasia, za kinguvu na utawala wao hunyima watu uhuru binafsi.

# JE KIONGOZI ANAPATIKANAJE?

*Kiongozi anaweza kupatikana kwa njia ya kuchaguliwa, kuteuliwa au kurithi;*

i. **Kuchaguliwa**
   Kiongozi hupigiwa kura na wananchi, ambapo watu mbalimbali wanaogombea uongozi hupigiwa kura.

ii. **Kuteuliwa**
   Kiongozi huteuliwa na mtu mwenye mamlaka kisheria pasipo kupigiwa kura. Mara nyingi mamlaka hayo hutoka katika ngazi za juu za uongozi.

iii. **Kurithi**
   Kiongozi hurithi nafasi kutoka kwa kiongozi aliyefariki au kuachia madaraka.



# SIFA ZA KIONGOZI

Kwa mujibu wa Katiba Ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977,Ibara ya 5(1) mtu yeyote bila kujali jinsia (mwanaume au mwanamke) mwenye umri usiopungua miaka 18 ana haki ya kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi (Ibara ya 5(1)).

**Ibara 39(1) ya katiba, imeweka sifa za mtu kuwa kiongozi kwa nafasi ya rais kama ifuatavyo:**

- Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Awe ametimiza umri wa miaka 40.
- Awe mwanachama wa chama cha siasa
- Awe na sifa za kumwezesha kuwa mbunge au mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.
- Hajawahi kutiwa hatiani katika mahakama yeyote kwa kipindi cha miaka 5 kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yeyote ya serikali.

**Ibara ya 67(1) ya katiba, imeweka sifa za mtu kuwa kiongozi kwa nafasi ya ubunge kama ifuatavyo:**

- Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Awe na umri usiopungua miaka 21
- Awe anajua kusoma na kuandika.
- Awe mwanachama wa chama cha siasa
- Hajawahi kutiwa hatiani katika mahakama yeyote kwa kipindi cha miaka 5 kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yeyote ya serikali.



**Kwa mujibu wa Mwongozo wa Uchaguzi wa Viongozi wa Ngazi za Vijiji, Vitongoji na Mitaa, Kifungu cha 10(1) sifa za mgombea zimeainishwa kama ifuatavyo:**

- Awe raia wa Tanzania;
- Awe na umri wa miaka 21 au zaidi;
- Awe anajua kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;
- Awe ana shughuli halali ya kumwezesha kuishi;
- Awe ni mwanachama wa chama cha siasa na amedhaminiwa na chama hicho;
- Hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano.
- Awe hana ugonjwa wa akili.

## Sifa nyingine za kiongozi ni pamoja na:

i. Awe mwenye utashi, busara na hekima
ii. Awe muaminifu, mkweli, mwenye msimamo
iii. Awe tayari kupokea mrejesho, anayejiamini na mwenye ushirikiano.
iv. Aweze kuwasiliana na mwajibikaji
v. Awe mkarimu na mvumilivu
vi. Aweze kusamehe

## JE WAJUA KWAMBA, WANAWAKE

1. Wana haki ya kuwa viongozi
2. Ni viongozi makini
3. Waaminifu na wenye msimamo
4. Huzingatia kuwa na sera za mahitaji ya kijinsia
5. Hutumia mamlaka yanayozingatia mahitaji kwa usawa wa kijinsia.
6. Hawana upendeleo wala ubaguzi
7. Ni viongozi bora na mfano wa kuigwa

# HALI YA USHIRIKI WA WANAWAKE KATIKA UONGOZI

Hali halisi ya ushiriki wa wanawake katika uongozi bado iko chini sana ukulinganisha na ushiriki wa wanaume:-
Katika ripoti ya Tamisemi ya uchaguzi wa serikali za mitaa ya mwaka 2014, inaonesha kama ifuatavyo;

- Wenyeviti wa mitaa waliochaguliwa ni 3,929. Kati yao, wanawake ni 435 tu.




- Wenyeviti wa serikali ya vijiji waliochaguliwa ni 12,275. Kati yao, wanawake ni 223 tu




- Wenyeviti wa vitongoji waliochaguliwa ni 64,691. Kati yao, wanawake ni 3,482 tu.



# JE NI KWANINI WANAWAKE HAWAJIHUSISHI NA UONGOZI?

Kuna sababu nyingi zinazopelekea wanawake wasishiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi kama ifuatavyo:

1. Fikra potofu na mitazamo hasi ilizojengeka katika jamii kuwa uongozi wa kisiasa ni nafasi za wanaume zaidi.
2. Kukosekana kwa utashi wa kisiasa katika vyama vya siasa kuweka mifumo shirikishi na rafiki unaowawezesha wanawake kushiriki katika nafasi za uongozi wa kisiasa.
3. Rushwa, hususan rushwa ya ngono
4. Baadhi ya imani za dini zinaamini kuwa wanawake hawawezi kuwa viongozi
5. Kutokujiamini na hivyo kukosa uthubutu kwa wanawake kujitokeza na kugombea
6. Ujuzi mdogo wa stadi za uongozi
7. Kukosa fursa za elimu
8. Majukumu mengi ya nyumbani
9. Kipato duni
10. Masuala ya ukatili wa kijinsia kwenye siasa (VAWP)
11. Wanaume wengi hawako tayari kuwaunga mkono wenzi wao kugombea nafasi za kisiasa.



# JE SHERIA ZINASEMAJE?

01

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara 21 (1) (2) inatoa fursa kwa raia wote kushiriki katika maswala yanayohusu uongozi nchini.
Ibara ya 12(1) inaeleza zaidi kuwa binadamu wote wamezaliwa huru na wote ni sawa.

02

Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 21(1),Sheria ya Vyama Vingi ya mwaka 1992 na Sheria ya Chaguzi za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 zinatilia mkazo juu ya haki za raia kushiriki katika harakati za kisiasa.

03

Katika ngazi za kimataifa, Tanzania imeridhia mikataba ya kimataifa inayosisistiza nchi wanachama kuchukua hatua kukuza uongozi shirikishi kwa wanawake na wanaume.

04

Mikataba ya kimataifa inayounga mkono ushiriki wa wanawake katika siasa ni pamoja na:

- Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu(UDHR 1948)
- Agano la Kitaifa juu ya Haki za kiraia na za kisiasa (ICCPR 1966)
- Agano la Kimataifa juu ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (ICESCR 1996)
- Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW 1979), NA Itifaki ya Hiari (Optional Protocol 1999).
- Mpango kazi wa Kimataifa Kuhusu Haki za Wanawake (Bijing Platform of Action 1995)
- Itifaki ya Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Binadamu na Watu juu ya Haki za Wanawake Afrika (2003)
- Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu Jinsia na Maendeleo (2008)
- Katiba, Sheria za Uchaguzi, Sheria ya Vyama Vya Siasa, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Jinsia na Wanawake.

# WAJIBU WETU NI NINI?

Elimisha jamii umuhimu wa uongozi shirikishi kati ya wanaume na wanawake.

Viongozi wa dini katika imani tofauti kuhamasisha waumini wao umuhimu wa kuwa na viongozi wanawake.

Pinga mila na tamaduni potofu zinazozuia ushiriki wa wanawake katika uongozi.

Shiriki katika harakati za kubadili mifumo kandamizi.

Tumia mamlaka ya pamoja ili kumwezesha mwanamke kushiriki.

Kemea lugha za udhalilishaji kwa wagombea wanawake.

Toa ruhusa kwa mwenza wako kushiriki katika uchaguzi.

Chagua viongozi wanawake watakaojitokeza kugombea nafasi mbalimbali.

Kuwa mmoja wa waleta mabadiliko yanayoamini katika usawa wa kijinsia.

Toa taarifa juu ya vitendo vya ukatili vinavyotokea wakati wa kampeni.

Shiriki katika kutimiza malengo ya asilimia 50% ifikapo 2030.

**Shiriki katika kutimiza malengo ya asilimia 50% ifikapo 2030.**



**Kimeandaliwa na kuchapishwa na:**
Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF)
Mikocheni "A" Area, Mtaa wa Chwaku/ Mtaa wa WiLDAF,
Block F, Plot No. 635, P. O. Box 76215, Dar es Salaam

**Simu:** 255 022 2701995
**BaruaPepe:** wildaftanzania@gmail.com | info@wildaftanzania.org
**Tovuti:** www.wildaftanzania.org **Mitandao ya Kijamii:** @willdaftz